**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

Mkoa wa Morogoro
Telegrams: "Afya Mkoa
Simu: 023-3099/4439
Email:moso@morogororrh.go.tz

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
Idara ya Afya
S.L.P.110


Unapojibutafadhalitaja:

**Kumb.Na.DC.176/262/08A/42**

**14/01/2026**

## TANGAZO LA NAFASI YA KUJITOLEA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro, inatangaza nafasi za kujitolea kwa kada mbalimbali kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kama ifuatavyo:

### 1. KADA- MTEKNOLOJIA DAWA (NAFASI – 7)

(a) **Sifa za Kuajiriwa**: wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia Dawa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na baraza pale inapohusika.

**MAJUKUMU**

(i) Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
(ii) Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi
(iii) Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
(iv) Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa
(v) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
(vi) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

### 2. KADA – AFISA MUUGUZI MSAIDIZI (NAFASI 2)

**Sifa za kuajiriwa**: wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kutoa huduma za uuguzi
(ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya.
(iii) uwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
(iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
(v) Kutoa huduma za kinga na uzazi
(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

## 3. KADA- DAKTARI II (NAFASI 6)

**Sifa za Kuajiriwa**: wenye Shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza "Internship" na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

**MAJUKUMU**

(i) Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.
(ii) Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa
(iii) Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.
(iv) Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement)
(v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

## A. SIFA ZA JUMLA KWA KAZA ZA AFYA

Waombaji wanatakiwa kuwa na:

i. Cheti cha taaluma cha kada aliyosomea cha chuo kinachotambuliwa na serikali.
ii. Awe amesajiriwa na baraza la kitaaluma
iii. Awe na leseni ya taaluma husika
iv. Awe na cheti cha kidato cha nne/sita kinachotambuliwa na NECTA
v. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 35
vi. Awe na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa umma
vii. Awe hajawahi kuhukumiwa na mahakama kwa makosa ya jinai
viii. Awe hajawahi kuajiriwa katika taasisi yoyote ya Umma tangu alipohitimu masomo.vc

## B. MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa za jumla kama ifuatavyo

i. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (cheti cha kidato cha nne, Sita, Taaluma na Usajili wa Kamili) "Full Registration" au Leseni hai ya kufanyia kazi ya taaluma husika.
ii. Maombi yaambatane na wasifu wa waombaji
iii. Maombi ya ambatishwe na nakala za vyeti vya elimu/taaluma na cheti cha kuzaliwa
iv. Testimonals result slip **HAITAKUBALIWA**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe** 02/02/2026

Maombi yatumwe kwa:

**Mganga Mfawidhi,**
**Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro**
**S.L.P 110,**
**Morogoro**

Imetolewa na:

Dkt. Daniel J. Nkungu
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MOROGORO**

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MOROGORO
S.L.P. 110
MOROGORO